

Je! Kutojali ni nini?

JAMII SALAMA KWA WATOTO

Kuna nyakati ambapo karibu wazazi wote hupata ugumu kukabiliana na mahitaji mengi ya kutunza watoto. Hii ni sehemu ya kawaida ya uzazi.

Wazazi wanatarajiwa kupeana upendo na utunzaji, usalama na chakula chenye afya, elimu, kuzingatia kimatibabu na usimamizi kwa watoto wao.

Ikiwa utakosa kupeana vitu hivi vya msingi kila wakati, basi huku ni **kutojali** na kuna sheria kuhusu hii nchini Australia.

Mwalimu, jirani au rafiki anaweza kuwa na wasiwasi kwa familia yako na wanaweza kuripoti kwa Idara ya Jamii, Huduma za Usalama wa Mtoto.

Ikiwa hii itafanyika, mfanyikazi kutoka kwa Huduma za Usalama wa Mtoto anaweza kuwasiliana nawe kuhusu familia yako.

Unaweza kushangaa au kuhisi kukasirika kwamba serikali inahusika katika maswala yako ya familia, lakini jaribu kuiona kama fursa ya kujua kuhusu sheria, kinachotarajiwa kutoka kwa wazazi nchini Australia na kupata msaada.

Omba mkalimani kila wakati ikiwa unahitaji mmoja. Ni haki yako kuelewa na kueleweka! Kutojali kunaweza kuwa na athari kali kwa ukuaji wa mtoto wako kimwili, kiakili na kihemko.

Hapa kuna mifano ya kutojali kuhusu usafi, chakula, afya, elimu na usimamizi.

Watoto huchafuka na hunuka pengine lakini ikiwa hii itatendeka kila wakati **hii inaweza kuwa kutojali**. Hii inaweza kuwa na athari mbaya kwa afya ya mtoto na masilahi yake ya kihemko.

Ni muhimu sana kwa watoto kuoga na kusugua meno na nywele zao kila siku.



Wanahitaji kuvaa nguo safi ambazo zinafaa hali ya hewa, na viatu visafi na soksi safi na watoto wakubwa wanapaswa kupaka manukato, wanapoenda shuleni.

Ikiwa mtoto wako hana chakula cha mchana shuleni na hii hufanyika kila wakati **hii inaweza kuwa kutojali**.

Wazazi wanatarajiwa kupeana chakula kwa watoto. Ni muhimu kupea mtoto wako kifurushi cha chakula cha mchana cha shule ambacho kinajumuisha chakula chenye afya kwa siku.

Ni sheria kwamba kila mtoto kuanzia miaka 6 hadi 15 lazima aende shule hapa Queensland.

Ikiwa mtoto wako anakosa kuhudhuria shule wakati mwingi bila sababu kupeanwa kwa waalimu au kuchelewa shuleni na hii inafanyika kila wakati, **inaweza kuwa kutojali.**

Ni muhimu kupanga asubuhi zako kuhakikisha watoto wako wanahudhuria na kufika shuleni kwa wakati unaofaa au wasiliana na shule ukiwa na sababu, ikiwa mtoto wako hayuko.

Ikiwa mtoto wako ni mgonjwa na hatunzwi vyema, **hii inaweza kuwa kutojali.**

Wakati mtoto wako ni mgonjwa, anapaswa kukaa nyumbani kutoka shuleni na ikiwa inahitajika aende kwa Daktari kwa msaada.



Wazazi wengi, haswa mzazi aliye peke yake, hupata ugumu kupanga kazi za kila siku na wanaweza kuacha watoto wadogo peke yao au chini ya ulinzi wa ndugu na dada wakubwa wanapoenda nje.

Usimamizi ni wajibu wa mzazi au mtu mzima na ikiwa watoto wataachwa nyumbani peke yao **hii inaweza kuwa kutojali.** Inaweza kuonekana kwamba unaweza watoto wako katika hatari kwa kuwaacha peke yao.

Ni hatari pia na kinyume cha sheria kuacha watoto wadogo peke yao katika sehemu za umma au kwenye gari.

Katika hali kadhaa unaweza kuhitaji kupanga rafiki, jirani au mtunzaji mtoto kukusaidia.

Uzazi unaweza kuwa mgumu na unaweza kuhitaji kuomba msaada wakati hauna familia yako kubwa karibu nawe.

Kuna baadhi ya mashirika yanayopeana mipango tofauti za uzazi kukusaidia kupata ustadi wa ziada katika kujisimamia wewe na familia yako.



Watoto wote wanastahili utoto salama, wenye afya na furaha.

Hapa kuna orodha ya baadhi ya sehemu ambazo zinaweza kukusaidia:

- **Huduma ya Mtafsiri wa Simu (TIS) Simu ya Kitaifa**
131 450 (masaa 24 kwa siku, siku 7).
- **Idara ya Huduma za Jamii za Usalama wa Mtoto**
1800 811 810
1800 177 135 (Baada ya Masaa ya kazi)
Hujibu hoja kuhusu maswala ya ulinzi wa mtoto wako
- **Kituo cha Utunzaji wa Kipeo QLD**
1800 177 135 (masaa 24)
Huduma ya jimbo zima ya ushauri wa simu na matatizo.
- **Kinections**
(07) 3435 4300
Shirika la msingi wa jamii linalotoa ushauri kwa watu kutoka asili ya wasiozungumza Kiingereza.
- **Laini ya Wazazi**
(07) 3369 1588 au 1300 30 1300 (8am – 10pm, yaani saa mbili asubuhi hadi saa nne usiku, siku 7)
Huduma ya ushauri wa simu kwa wazazi
- **Huduma ya Afya ya Jamii ya Mtoto**
1800 177 279 (Laini ya Afya ya Mtoto — masaa 24, siku 7 kwa wiki)
13 Health
- **Laini ya Kuwasaidia Watoto**
1800 551 800
Ushauri wa simu kwa vijana wenye umri wa kati ya miaka 5 na 25.
- DVD ya 'Kumlea Watoto nchini Australia; kwa wazazi wa watoto wadogo nchini Australia' (katika lugha 10 za Afrika) inapatikana bure kutoka kwa **Idara ya Familia na Jamii na Maswala ya Watu wa Asili (FaHCSIA)**
1800 050 009



This document was developed by Multicultural Development Association (MDA) with funding from the Australian Government Department of Families, Housing, Community Services and Indigenous Affairs (FaHCSIA)